



Kelvin R. Adams, Ph.D.
Superintendent of Schools



Agosti 16, 2017

FAMILIA ZA SLPS:

Tunatarajia familia yako ilikuwa na majira mazuri. Tunawangojea watoto wenu kwa hamu wakirejea katika kumbi na madarasa.

Jumatatu, Agosti 21, tutaadhimisha kupatwa kwa jua katika wilaya yote. Huu ni wakati mmoja katika maisha unaoweza kuwa muhimu kielimu, na wataalamu wetu wa taaluma za kisayansi wamekuwa wakijiandaa katika shughuli za kujifurahisha na elimu. Kila mwalimu amekamilisha kikao kina cha maendeleo ya kitaaluma kuhusu kupatwa kwa jua na usalama wa tukio hili. Maelezo yametayarishwa kwa kila kikundi kulingana na umri. Miwani za usalama zimeagiziwa kila mwanafunzi na kila mfanyakazi wa shule. Tuko tayari!

Tunakuhimiza kuja shule ya mtoto wako siku hiyo na kufurahia tukio hilo na watoto wako. (Tafadhali uje na miwani ya usalama kwa sababu hatutakuwa na ziada.) Tunatarajia ujiunge na sisi kwa tukio hili la kipekee.

Kadhalika tunatoa njia kwa ajili ya familia ikiwa hawataki mtoto wao nje wakati wa kupatwa kwa jua. Wanafunzi hawa wataangalia mkondo wa NASA ndani ya jengo la shule. Unaweza kuchagua kujiondoa hapa: www.slps.org/NoEclipse au unaweza kujaza toleo la karatasi (iliyoshikanishwa) na mtoto wako airudishe shulenii jumatatu kabla ya asubuhu kuisha.

Unaweza kupata maelezo zaidi juu ya kupatwa kwa jua kwenye www.slps.org/Eclipse. Asante kwa kuchagua Shule za Umma za Saint Louis kwa watoto wako. Tunatarajia mwaka wa shule ya 2017-2018 mwema!

Kwa uaminifu,

A handwritten signature in black ink, appearing to read "Kelvin R. Adams".

Kelvin R. Adams, PhD
Superintendent of Schools
Saint Louis Public Schools